**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

# HOTUBA YA MHESHIMIWA DKT. PHILIP ISDOR MPANGO, MAKAMU WA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, WAKATI WA UZINDUZI WA MAONESHO NA SHEREHE ZA WAKULIMA, WAFUGAJI NA WAVUVI - NANENANE,

**VIWANJA VYA JOHN MWAKANGALE, MBEYA**
**01 AGOSTI 2022**

- ***Mheshimiwa Hussein M. Bashe (Mb), Waziri wa Kilimo;***
- ***Mheshimiwa Mashimba M. Ndaki (Mb), Waziri wa Mifugo na Uvuvi;***
- ***Waheshimiwa Naibu Mawaziri;***
- ***Wawakilishi wa Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa (Songwe, Katavi, Ruvuma, Njombe na Iringa) mkiongozwa na Mheshimiwa Dkt. Rashid Chuwachuwa Kaimu Mkuu wa Mkoa wa Mbeya;***
- ***Waheshimiwa Wabunge kutoka Kanda hii ya Nyanda za Juu Kusini;***
- ***Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu wa Wizara wote mliopo;***
- ***Komred Jacob Mwakosole, Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Mkoa wa Mbeya;***
- ***Viongozi wa Vyama Shindani – Nimemuona Joseph Mbilinyi (a.k.a Sugu);***
- ***Mheshimiwa Sheduro Mohammed, Mstahiki Meya wa Jiji la Mbeya;***
- ***Viongozi wetu wa Dini (Bwakata, TEC, CCT) na Viongozi wote wa Serikali na Taasisi za Uma mliopo;***
- ***Kamati ya Ulinzi na Usalama Mkoa;***
- ***Wadhamini wote wa Maonesho haya;***
- ***Wakulima, Wafugaji, Wavuvi na Wanaushirika;***
- ***Ndugu Wanahabari;***
- ***Kwaya ya Utumishi; Brass Band; Agano Kwaya; Peter Msechu; na Vijana wa Hamasa;***
- ***Ndugu Wananchi, Wageni waalikwa, Mabibi na Mabwana.***

**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania…**

**Maonesho ya Nanenane Oyee!  Mbeya oyee!**

Waheshimiwa Viongozi, Wananchi na wageni waalikwa, napenda nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na kutukutanisha

hapa Jijini Mbeya, ili kuzindua rasmi maonesho ya 29 ya Nanenane kitaifa kwa mwaka 2022. Aidha, napenda niwashukuru wananchi wa Jiji la Mbeya na mikoa ya jirani kwa kujitokeza kwa wingi katika uzinduzi huu katika viwanja hivi vya John Mwakangale. **Asanteni sana!**

Kipekee, napenda kuleta kwenu salamu za Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Anawapongeza sana wakulima, wafugaji, wavuvi na wanaushirika wa mikoa yote nchini na hususan wa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini kwa kazi nzuri ya uzalishaji wa mazao ya kilimo, mifugo, uvuvi na misitu unaotuwezesha kuwa na uhakika na usalama wa chakula na kipato. Anawasihi mwendelee kuchapa kazi kwani sekta ya kilimo kwa upana wake ni uti wa mgongo wa uchumi wa taifa letu. Aidha, anawatakia wadau wote wa sekta za kilimo, mifugo, uvuvi na misitu mafanikio katika Maonesho haya adhimu yanayofanyika katika kanda zote nchini kuanzia siku hii ya leo hadi yatakapofungwa siku ya Nanenane, tarehe 8 Agosti, 2022.

Napenda pia kutoa shukrani kwako Mheshimiwa Waziri wa Kilimo **na Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi** kwa kunialika kushiriki katika uzinduzi wa Maonesho haya. Nafurahi sana kuwa hapa kwani hata mimi ni mdau na mkereketwa wa kilimo cha mazao na ufugaji wa wanyama, samaki, kuku na nyuki; pamoja na uongezaji thamani. Vilevile, napenda kuushukuru uongozi wa mkoa wa Mbeya; Kamati ya Maandalizi; Wizara za Kilimo, Mifugo na Uvuvi na Wizara nyingine za Kisekta; Wakuu wa Mikoa ya Njombe, Iringa, Rukwa, Ruvuma, Katavi na Songwe; pamoja na wadau wote, kwa maandalizi mazuri ya maonesho haya. **Hongereni sana!**

***Waheshimiwa Mawaziri, Viongozi wote mliopo,***
***Ndugu Wananchi, mabibi na mabwana***

Maonesho haya ni fursa adhimu kwa wadau wote kwenye sekta za kilimo, maliasili, ufugaji na uvuvi. Nafurahi kuona wananchi kutoka mikoa mbalimbali, mmejitokeza kwa wingi kushiriki na kutembelea mabanda yaliyopo ili muweze kunufaika na maonesho haya. Nimepata fursa ya kutembelea mabanda na kujionea shughuli mbalimbali zinazohusiana na teknolojia ya uzalishaji na usindikaji wa mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi. Pia, nimeona shughuli mbalimbali zinazofanywa na wanaushirika na wajasiriamali ambazo ni chachu katika kuendeleza kilimo, misitu, mifugo na uvuvi. Naomba nikiri kwamba teknolojia na fursa mbalimbali za kuongeza tija nilizozishuhudia katika sekta hizi za kilimo, misitu, uvuvi na ufugaji zimenipa hamasa kubwa. Nina imani kwamba wananchi wote tutaendelea kujifunza mengi kupitia maonesho haya

ili yatusaidie kuboresha shughuli zetu za kilimo, ufugaji, uvuvi na biashara ya bidhaa za kilimo na misitu.

***Ndugu Viongozi, Wananchi na wageni waalikwa***

Sote tunatambua kuwa Sekta ya Kilimo ni mhimili muhimu katika kukuza uchumi wa Taifa letu na kuleta maendeleo kwa wananchi. Katika Mwaka 2021, Sekta ya Kilimo ilichangia takriban robo ya pato la Taifa (26%). Sekta ya mazao, peke yake inachangia asilimia 14.6 katika Pato la Taifa, na inachangia zaidi ya asilimia 100 ya mahitaji ya ndani ya upatikanaji wa chakula. Kwa upande wa sekta ya mifugo na uvuvi, sekta ya mifugo inachangia asilimia 7 katika Pato la Taifa wakati sekta ya uvuvi inachangia asilimia 1.8. Aidha, sekta hii ya kilimo ni sekta inayotoa ajira kuliko sekta zote hapa nchini (asilimia 61.1). Vilevile sekta hii inachangia asilimia 65 ya malighafi za viwandani. **Kilimo, Mifugo na Uvuvi oyee!**

Kwa kutambua umuhimu wa sekta hizi, Serikali inaendelea kuboresha na kuendeleza sekta ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi. Kwa mfano, ili kutatua changamoto zilizopo kwenye kilimo, mifugo na uvuvi, Serikali imeongeza bajeti ya Kilimo kutoka shilingi bilioni 294 mwaka 2021/2022 hadi shilingi bilioni 751.1 mwaka 2022/2023; na Mifugo kutoka shilingi bilioni 47.8 mwaka 2021/2022 hadi shilingi bilioni 52 mwaka 2022/2023. Katika bajeti hizo, baadhi ya maeneo ya kipaumbele yaliyoongezewa fedha ni pamoja na Utafiti; Huduma za ugani; Umwagiliaji; Udhibiti wa magonjwa; Uzalishaji wa mbegu; Ujenzi wa miundombinu ya uhifadhi na masoko; ukuzaji wa viumbe maji, uchumi wa buluu; na miradi mipya yenye lengo la kuhusisha vijana (*Building a Better Tomorrow* - BBT).

***Ndugu Viongozi, Wananchi na Wageni Waalikwa;***

Tunatambua upatikanaji wa pembejeo kwa wakati umekuwa ni kikwazo kikubwa katika maendeleo ya kilimo. Tatizo hili limekuzwa zaidi na mlipuko wa UVIKO-19 na vita vya Urusi na Ukraine ambavyo vimeathiri mfumo wa uzalishaji wa pembejeo hizo. Napenda niwahakikishie kuwa Serikali inaendelea kujipanga vizuri kukabiliana na changamoto hiyo. Kwanza, tumeanza kujenga uwezo wa ndani wa kuzalisha mbolea ya kutosha ambapo tumepata mwekezaji mkubwa wa mbolea huko Nala Dodoma. Kiwanda hiki pamoja na kile cha Minjingu vinatarajiwa kuleta unafuu mkubwa katika upatikanaji wa mbolea nchini. Hatua nyingine, ni kuanzishwa kwa Mfuko wa Mbolea ambapo tayari Wizara ya Kilimo imeshatenga shilingi bilioni 150 ili kuanza kutoa mbolea ya ruzuku. Zoezi la usajili wa wakulima, waagizaji wa mbolea na mawakala limeshaanza kutekelezwa. Aidha, Serikali inarejesha mfumo wa

manunuzi ya mbolea kwa pamoja (Bulk Procurement System) ambao utapunguza mlolongo wa upatikanaji wa pembejeo.

***Ndugu Wananchi;***
Napenda nitumie fursa hii kusisitiza masuala muhimu yafuatayo:

**Jambo la Kwanza,** ni kuhusu changamoto kubwa ya mabadiliko ya tabianchi. Athari za mabadiliko ya tabianchi, kupotea kwa uoto wa asili na uchafuzi wa mazingira hivi sasa ni changamoto ambazo zinahatarisha uzalishaji wa mazao, mifugo na hata upatikanaji wa samaki. Sote ni mashahidi kuwa mwaka huu baadhi ya mikoa yetu haikupata mvua za kutosha tofauti na ilivyo kawaida. Kadhalika, mwaka uliopita baadhi ya mikoa yetu ilikuwa na vipindi virefu vya ukame vilivyosababisha vifo vya mifugo mingi. Aidha, katika baadhi ya maeneo kulikuwa na mafuriko. Haya yote ni matokeo hasi ya mabadiliko ya tabianchi ambayo yanaathiri uzalishaji katika sekta zetu za kilimo, uvuvi, mifugo na maliasili. Rai kwa wafugaji: **Tunzeni vyanzo vya Maji! Tukiharibu sehemu moja tunahama lakini tunakohamia pia tunaharibu lazima wafugaji tuwe walinzi wa vyanzo vya maji.**

Kwa mantiki hiyo, ni wajibu wetu kutunza mazingira yetu na kupanda miti kwa wingi ili kuepuka athari zaidi. Vilevile, kupitia hadhara hii nazikumbusha tena Halmashauri zote nchini kuwa na mpango wa matumizi bora ya ardhi ambao utaainisha maeneo kwa ajili ya shughuli za kilimo, misitu, mifugo na uvuvi. **Aidha, Halmashauri zitenge bajeti kwenye mipango yao kusaidia Maafisa Mifugo kwenda kutoa huduma za ugani kwa Wafugaji.**

**Jambo la Pili,** ni kuhusu usimamizi wa Maafisa Ugani: Katika ziara zangu mikoani nimekuwa nikipokea malalamiko mengi ya wananchi kuhusu ukosefu wa huduma za ugani! Ni jambo la kweli maana hata mimi Makamu wa Rais sitembelewi na wataalam wa kilimo, mifugo na samaki shambani kwangu Dodoma! Hata watafiti wa TARI siwaoni! Mheshimiwa Waziri wa Kilimo unafahamu kasoro hii. Licha ya ahadi na jitihada za Serikali kusomesha na kuajiri Maafisa Ugani na kuwapatia vitendea kazi, ni lazima pia kazi za maafisa hawa zisimamiwe ipasavyo. Muda umefika sasa kwa TAMISEMI kushirikiana na Wizara za sekta za kilimo, misitu, mifugo na uvuvi kuweka utaratibu wa kupima matokeo ya huduma wanazotoa Maafisa Ugani. Hawapaswi kukaa maofisini wala kuvaa suti wakati wakiwa kazini! Hali kadhalika, Maafisa Ugani wenyewe hawana budi kuwa na mashamba darasa ili waweze kutoa elimu kwa vitendo na sio nadharia tu. Hili ni jambo muhimu ili kuleta motisha na hamasa kwa wakulima na wafugaji wetu na pia kuongeza tija. **Ninaitaka Ofisi ya Waziri Mkuu kuweka mfuko utakaowezesha Wizara**

**kusimamia na kufuatilia utendaji wa Wataalamu wa Sekta zao walioko katika Halmashauri**.

**Jambo la Tatu,** napenda kuziagiza taasisi zetu za utafiti kujiongeza na kutafiti mbegu ambazo zinazaa zaidi na mazao mapya yanayostawi vizuri katika kila mkoa. Tuachane na mazoea kwamba katika mkoa fulani zao hili au lile halistawi bila kujaribu. Mfano parachichi, komamanga na karangamiti zinaweza kustawi Dodoma na siyo tu mtama, alizeti, zabibu na mazao mengine yaliyozoeleka. Lakini pia kwenye upande wa teknolojia napenda nihimize taasisi zetu za umma na binafsi kuweka nguvu zaidi katika kubuni mashine kwa ajili ya kusindika na kuongeza thamani ya mazao na bidhaa mbalimbali tunazozalisha. **Mheshimiwa Rais ameongeza fedha za utafiti na uzalishaji wa mbegu. Wizara za Kilimo, Mifugo na Uvuvi hakikisheni zinatumika kama ilivyokusudiwa. Maeneo yapewe hati za umiliki na yazungshiwe uzio. Viongozi wa Taasisi hizi nao wafanye kazi kweli kweli tuone mabadiliko na tija.**

**Jambo la Nne,** ni uhaba wa malighafi na vifungashio. Changamoto hii inawakabili zaidi wenye viwanda na wajasiliamali. Viwanda vyetu vingi vinazalisha chini ya uwezo kutokana na upungufu wa malighali na vifungashio ambavyo vinauzwa kwa bei kubwa, baadhi havina ubora na pia havipatikani kwa urahisi. Hivyo napenda kuwakumbusha tena Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara pamoja na Sekta Binafsi kushughulikia hili. Ninaelekeza Wizara za Uwekezaji, Viwanda na Biashara; Kilimo; Mifugo na Uvuvi; na Maliasili kufanya jitihada kubwa ili pamoja na mengine, kuelewa mwenendo (*dynamics*) wa masoko ya mazao, ikiwemo taratibu ya kuchumbia katika ununuzi wa mazao (*forward buying and selling*), vipimo vinavyotumika ikiwemo lumbesa, uendeshaji wa maghala ya nafaka na mazao mengine, udhibiti wa ubora na upangaji bei kwa njia ya kuhodhi masoko na hivyo kuwakandamiza wakulima masikini na kuchukua hatua stahiki kuwanusuru wakulima wetu. **Mheshimiwa Waziri wa Kilimo amezungumza hapa jinsi Lumbesa inavyowanyonya wakulima wetu na pia kuikosesha Serikali mapato. Sasa naagiza kwamba Lumbesa hapana! Mazao (viazi, vitunguu, mpunga) yauzwe kwa kutumia vipimo sahihi (mizani) katika mikoa yote hapa nchini. Wakuu wa Mikoa na Wilaya wote msimamie hili. Uuzaji wa mifugo pia utumie vipimo sahihi. Mizani itumike kwenye minada.**

**Jambo la Tano,** kuhusu changamoto ya kukosekana kwa njia bora ya kuhifadhi mazao ya kilimo. Nafahamu kuna baadhi ya mazao yetu huharibika haraka shambani na kabla ya kufika sokoni na wakati mwingine mkulima kulazimika kuuza kwa bei ya hasara kabla ya mazao kuharibika. Katika hili,

napenda kusisitiza na kuelekeza Vyuo na Taasisi zetu za Umma kama DIT, SIDO, TEMDO nk. na Taasisi Binafsi kubuni teknolojia rafiki ya kuhifadhi na kusindika mazao ya biashara ili kuepuka uharibifu wa mazao yasiyoweza kuhifadhiwa kwa muda mrefu. Vilevile, naiagiza Wizara ya Kilimo kushirikiana na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi na TAMISEMI kuendelea kujenga majokofu ya kuhifadhia mazao ya kilimo yanayoharibika haraka kwenye viwanja vyetu vya ndege na masoko (*cold rooms*). Aidha, natoa wito kwa sekta binafsi kuanzisha viwanda vidogo vidogo vya kusindika mazao hasa haya yanayo haribika haraka. Wizara za Kilimo, Mifugo na Uvuvi pamoja na Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kupitia Kituo cha Uwekezaji Tanzania, waweke nguvu zaidi kuvutia wawekezaji wa kuchakata na kuongeza thamani ya mazao yanayolimwa au kuzalishwa kwa wingi katika Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini na mikoa mingine kama mahindi, maharage, kahawa, chai, parachichi, ndizi, viazi, ufuta, korosho, pareto, mazao ya mifugo, samaki na mazao ya misitu.

**Jambo la Sita,** Ili tuweze kufanikiwa kufanya kilimo kuwa cha kibiashara ni lazima kuwa na masoko ya uhakika. Tunapolima, tunapovua samaki, tunapochinja au kukamua maziwa ni lazima kujua tunapeleka wapi mazao yetu. Hivyo naziagiza Wizara za kisekta zinazohusika kushirikiana na Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara pamoja na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kutafuta na kupanua wigo wa masoko ya bidhaa zetu. Aidha, natoa rai kwa Viwanda vyetu, kuendelea kununua malighafi zinazotokana na mazao ya kilimo yanayozalishwa hapa nchini ili kusaidia wakulima wetu kuwa na masoko ya uhakika.

**Jambo la Saba,** kama nilivyoeleza hapo awali, mwaka huu mvua hazikuwa za kuridhisha katika nchi yetu. Hivyo ni muhimu kuchukua tahadhari. **Pamoja na maelezo mazuri ya Waziri wa Kilimo**, nazihimiza kaya zote kujiwekea akiba ya chakula. **Wafugaji wapunguze mifugo kwa kuiuza kipindi hiki ambapo kuna soko zuri na watumie fedha hizo kujiwekea akiba ya chakula na shughuli nyingine za maendeleo**. Na kwa upande wa Serikali nawakumbusha, Wizara ya Kilimo, Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) na Bodi ya mazao mchanganyiko kufuatilia na kufanya tathmini ya hali ya chakula nchini na kuhakikisha nchi inabaki kuwa na akiba ya chakula cha kutosha. Bahati nzuri katika eneo hili la hifadhi ya chakula Mheshimiwa Rais ameongeza fedha hadi kufikia bilioni 119 mwaka 2021/22, ambazo ni zaidi ya mara sita ukilinganisha na bajeti ya mwaka 2020/21.

**Jambo la Nane**, napenda kutoa rai kwa taasisi za fedha kuendeleza jitihada za kuweka masharti nafuu ya upatikanaji wa mikopo kwa wakulima, wafugaji

na wavuvi **na kuzitangaza** ili kuongeza uwekezaji na uzalishaji katika sekta hizo na kupunguza changamoto za ajira. **Ni kweli benki zetu hasa NMB na CRDB zimechukua hatua. Niliwaomba mpunguze riba za mikopo kwa wakulima, wafugaji na wavuvi. Mmeishia 9% wote! Nawapongeza lakini bado.** Aidha, napenda kuelekeza Shirika la Bima la Taifa na benki zetu kuweka nguvu zaidi kuelimisha wakulima, wafugaji na wavuvi kuhusu huduma na faida ya kuwa na bima ya mazao. **Ninaitaka Benki Kuu ya Tanzania itazame upya sheria za kifedha na kanuni zinazokwamisha wawekezaji katika kilimo biashara (hasa wazalendo).**

**Jambo la Tisa**, Kumekuwa na taarifa ya kushuka kwa biashara kati ya Tanzania na baadhi ya majirani zetu katika Ukanda wa Nyanda za Juu Kusini licha ya kuwa na Bandari inayotuwezesha kupata bidhaa hizo kwa gharama nafuu na jitihada za Benki Kuu kupunguza gharama na kurahisisha ubadilishanaji wa bidhaa mipakani. Naagiza Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango kupitia taasisi zenu za Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Bodi ya Biashara ya Nje (BET), kubaini ukubwa na kiini cha wafanyabiashara wa Tanzania katika mikoa ya mpakani, kuhamishia biashara zao upande wa baadhi ya nchi jirani katika Ukanda huu, na baadhi ya wafanyabiashara wa nchi jirani kupitishia bidhaa katika nchi nyingine jirani badala ya moja kwa moja kutoka Tanzania.

**Na mwisho,** napenda nitumie hadhara hii kuwaomba wasomi wetu hususan vijana waliosomea kilimo kuingia katika sekta ya kilimo badala ya kusubiri kuajiriwa na Serikali. Hakika *Kilimo biashara kinalipa!* **Mabanda niliyotembelea Wakulima, Wafugaji na Wavuvi wameshuhudia hili**. Vivyo hivyo, nawahamasisha viongozi na wafanyakazi Serikalini kuingia pia katika sekta hizi za kilimo, ufugaji na uvuvi. Sisi viongozi tukishiriki katika kilimo, itatusaidia kuelewa changamoto za kilimo kwa uhalisia zaidi na hivyo kuzitatua kulingana na mazingira. Aidha, nawaomba watanzania wote kwa ujumla, tukipende na kukiheshimu kilimo kwa sababu ni kazi kama zilivyo kazi nyingine. Tulio wengi, tulisomeshwa na wazazi wetu kwa kutegemea kilimo, biashara ya mazao, ufugaji na uvuvi na mpaka sasa shughuli hizo zimeendelea kubaki kuwa tegemeo la familia zetu nyingi.

***Ndugu Viongozi, Wananchi na Wageni waalikwa***

Kabla sijamaliza Hotuba yangu naomba nizungumzie kidogo kuhusu hali ya miundombinu ya wenyeji wetu Mkoa wa Mbeya. Serikali ya awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan imesikia kilio cha wana Mbeya hususan kuhusu barabara inayoingia katika jiji kuelekea Songwe kuwa

ni nyembamba na ina msongamano wa magari makubwa yanayoelekea nchi Jirani. Napenda kuwathibitishia tena wananchi wa Mbeya kuwa Serikali itajenga Barabara ya njia Nne (29 Km) kuanzia Uyole (Nsalaga) hadi Ifisi na na zabuni ya ujenzi wa barabara hii umeshatangazwa. Aidha, Serikali itajenga barabara ya mchepuko kutoka Uyole hadi Songwe (Km 48.9) itakayowezesha magari makubwa ya mizigo kupita kwenda nchi Jirani na mikoa inayopakana na Jiji la Mbeya.

Vilevile, Serikali imesikia kilio cha wananchi wa Mbeya Mjini **kupitia kwa Mbunge wao makini Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** kuhusu barabara inayotoka barabara Kuu ya kwenda uwanja wa ndege wa zamani ambapo kwa sasa kuna kero kubwa ya vumbi na wakati wa mvua ni tope. Napenda niwajulishe kuwa barabara hiyo sasa itajengwa kwa kiwango cha lami ili kuwawezesha wananchi kufika katika eneo jipya la wafanyabishara ndogondogo kwa urahisi zaidi. Ofisi ya Rais TAMISEMI kupitia TARURA watafute fedha na ujenzi wa barabara hiyo uanze mwaka huu wa fedha.

***Ndugu Viongozi, Wananchi na Wageni waalikwa***

Napenda nihitimishe hotuba yangu kwa kuendelea kusisitiza kuwa tarehe 23 Agosti mwaka huu nchi yetu itaendesha zoezi la sensa ya Watu na Makazi. Hivyo, nawaomba wananchi wote tujitokeze kuhesabiwa. Aidha, sensa ya mwaka huu ni ya kipekee kwani kwa mara ya kwanza itakusanya taarifa za makazi. Napenda nitoe wito kwa wananchi wote kutoa ushirikiano wa dhati kwa wataalam wanaohusika na zoezi hilo ili lifanyike kwa ufanisi kwa ajili ya kutusaidia kupata takwimu sahihi za idadi ya watu kwa maendeleo. Nawasihi tusifiche idadi sahihi ya watoto, watu wenye ulemavu, wazee, wanawake, wanaume na kaya wanapoishi.

Baada ya kusema hayo, sasa ninayo heshima kutangaza kwamba **Maonesho na Sherehe za Wakulima, Wafugaji na Wavuvi - Nanenane 2022 yamezinduliwa rasmi.**

**Mbeya Oyee!**
**Asanteni sana kwa kunisikiliza.**